**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI**

# FOMU YA KUJIUNGA NA SHULE

## SHULE YA SEKONDARI YA LINDI WASICHANA (LINDI GIRLS)

Bi. ______________________________,
______________________________,
______________________________,

**MAELEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI LINDI WASICHANA HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI, MKOA WA LINDI MWAKA 2023.**

1. Karibu **SHULE YA SEKONDARI LINDI WASICHANA**
2. Awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza kwa kuchaguliwa kujiunga kidato cha tano katika shule hii. Jumuiya ya Shule ya Sekondari Lindi Wasichana (**LINDI GIRLS SECONDARY SCHOOL)** tunasema HONGERA NA KARIBU LINDI.

**UTANGULIZI**

Shule ya Sekondari Lindi Wasichana ni miongoni mwa shule mpya 10 zilizojengwa na **Serikali ya Awamu ya Sita** katika mikoa 10 ya Tanzania Bara. Shule ni ya bweni **maalum ya sayansi** kwa **wanafunzi wa kike**. Shule hii ina mandhari na mazingira mazuri ya kufundishia na kujifunzia.

Shule itafunguliwa tarehe 14 Agosti 2023 na wanafunzi wote wanatakiwa kuripoti tarehe 13 Agosti 2023 kabla ya saa 11 jioni.

Ni mategemeo yetu utafurahia maisha kwa muda wote utakaosoma hapa na kwamba utaonyesha tabia njema, utakuwa na ari ya kujifunza na utajitahidi, kutekeleza shughuli zote zinazomhusu mwanafunzi kwa juhudi na maarifa.

Walimu, Wafanyakazi, Wanafunzi wenzako na wanajumuiya wote kwa ujumla wapo tayari kukupa kila msaada utakaohitaji.

Shule ya Sekondari Lindi Wasichana iko umbali wa mita 800 kutoka barabara kuu ya Lindi - Dar es saam, Mtaa wa Kilangala B, na ipo umbali wa kilometa 40 kutoka Lindi Mjini. Ili uweze kufika shuleni kwa urahisi kutokea Dar es Salaam, panda mojawapo ya mabasi yaendayo Lindi, Mtwara, Masasi, Newala, Nachingwea, Ruangwa, Tunduru au Songea, shuka mtaa wa Kilangala (KM 40 kabla hujafika Lindi Mjini). Wanafunzi wanaotokea Lindi, Mtwara, Newala

Masasi, Tunduru na Songea wapande mabasi yaendayo Dar es Salaam na watelemke Mtaa wa Kilangala (KM 40 baada ya Lindi Mjini). Aidha kutoka standi ya Kilangala hadi shuleni kuna umbali wa mita 800, ambapo mwanafunzi anashauriwa kutumia usafiri wa pikipiki hadi shuleni kwa Tshs 1,000/

Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **13/8/2023** bila kukosa kwa ajili ya kuanza muhula wa kwanza wa masomo. Mwanafunzi atakayechelewa kuripoti bila taarifa yoyote nafasi yake itachukuliwa na mtu mwingine baada ya wiki 2 toka shule ilipofunguliwa.

**NB.**

**Tafadhali kama umepata shule sehemu nyingine na hutaripoti, toa taarifa shuleni hapa kwa barua ili Wizara ifanye utaratibu wa kumpa nafasi mwanafunzi mwingine.**

## 3. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:

### i. Sare ya Shule

*(a)* *Mwanafunzi aje na sketi mbili za* ***Dark Blue,*** *kwa muonekano ufuatao:*

- Sketi zake ziwe ndefu kutoka kwenye kisigino mpaka kwenye pindo la sketi zisizidi sentimeta 18 au inchi 7½.
- Sketi zake zisiwe na (belt) mkanda mpana, upana wa belt usizidi sentimeta 05 au inchi moja na nusu.
- Ziwe na marinda mawili mbele yanayo tengeneza V, Sketi isibane iwe na upana wa kutosha . Mchoro wa mshono wa sketi umeambatanishwa na barua hii.
- Mzazi/mlezi na mwanafunzi tafadhali zingatia vipimo hivyo, mwanafunzi atakayeshona na kuja na sketi/shamba dress kinyume na vipimo, rangi na aina ya kitambaa tulichoelekeza hatapokelewa, atarudishwa nyumbani ili aje na sare zilizoelekezwa.

(b) Shati (blauzi) nyeupe mbili (2) za mikono mifupi - tetroni

(c) Viatu vyeusi (**visiwe na visigino virefu (high heels**) jozi mbili (02) au zaidi

(d) Soksi nyeupe jozi mbili (2) au zaidi.

(e) Bukta nyeusi kwa ajili ya michezo
isiwe na urembo wowote.

(f) Raba nyeupe kwa ajili ya michezo

(g) Truck Suit dark blue isiyobana kwa ajili ya maandalizi ya jioni.

(h) T-shirt 1 ya rangi ya Blue ya round

(i) Shamba dress 2-Light Blue (Blue Bahari) – gauni lililoshuka chini mchoro umeambatishwa na barua hii.

(j) Sweta moja dark blue

***NYONGEZA****: Kwa wanafunzi wa Kiislamu: Vazi la Msikitini*

- Suruali nyeusi ya heshima na isibane
- Blauzi nyeusi ndefu ipite magoti na yenye mikono mirefu.
- Hijabu ya tetroni nyeupe/juba na sio mtandio, isiwe na urembo wowote. Pia isiwe na urembo wa lessi.

***ANGALIA:*** Mzazi/mlezi wa mwanafunzi kama unadhani itakuwa vigumu kufuata utaratibu/vipimo, mwanao anaweza kuja na fedha na atashonewa hapa shuleni kwa gharama hizi hapa chini.

Mwanafunzi anaweza kushona sare mbili (2) au zaidi. Inashauriwa awe na angalau sare za darasani mbili na gauni za kazi mbili.

Sare ya shule ni kama ilivyoelekezwa katika maelekezo. Mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare wakati wote wa masomo, na anapokwenda hospitali, mjini au anapokuwa katika shughuli zozote za kishule nje ya eneo la shule. Ni marufuku kabisa kujipamba wakati amevaa sare ya shule akiwa shuleni.

## 4. MAHITAJI MUHIMU KWA MWANAFUNZI.

i. Awe na sanduku (nunua sanduku la bati) linalofunga vizuri kwa kuhifadhia nguo na vitu vyake.
ii. Aje na godoro 01 la futi 3x6
iii. Aje na Mto na Foronya yake
iv. Blanket moja la futi 3 x 6
v. Aje na bed cover (shuka moja) ya pink bahari futi 3 x 6 na foronya ya blue bahari visivyo na maua au urembo wowote.
vi. Shuka za Kulalia mbili za futi 3 x 6 rangi ya Pink.
vii. Taulo za kike za kutosha
viii. Taulo la bafuni
ix. Koti la mvua au mwavuli
x. Kandambili kwa ajili ya kuogea.
xi. Viatu vya plastiki (yebo) rangi yoyote vya kushindia.
xii. Aje na kifaa kimoja kulingana na mkondo wake, kama ilivyobainishwa hapo chini:

**Tahasusi ya PCB - Kwanja na Reki,**

**Tahasusi ya CBG - Jembe,**

**Tahasusi ya PGM - Panga**

- Soft broom moja (01).
- Hard broom moja (01)
- Mfagio wa kukaushia maji (drier) (01)
- Ndoo ndogo mbili (moja kwa matumizi ya shule na nyingine kwa matumizi yake binafsi bwenini).
- Fagio la chelewa moja (01)
- Brush ngumu (1) ya kusugulia choo yenye mpini mfupi wa mbao/mti kwa ajili ya kusafishia sinki la choo.
- Alete container lenye mfuniko/sahani, bakuli,kikombe na kijiko
- Daftari (Kaunta books) quire three zisizopungua kumi (10)
- Picha pasport size 4
- Ream moja ya karatasi A4 (photocopy paper) kila muhula

- Mathematical set moja (01) kwa matumizi yake awapo darasani.
- Scientific Calculator kwa wanafunzi wanaosoma **MATHEMATICS**
- Graph pad moja (1) kwa mwaka
- Alete chandarua/Net - futi 3 x 6.
- Dissecting kit (kwa wanaosoma Biolojia).
- Koti la maabara jeupe kwa wanafunzi wote

## 5. MICHANGO MINGINE:

| Na. | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 2. | Tahadhari | 5,000/= |
| 3. | Nembo | 5,000/= |
| 4. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

## 6. FEDHA ZA MATUMIZI

Mzazi unashauriwa kumpatia fedha za matumizi binafsi ya mwanafunzi kulingana na tamaduni za kitanzania.

## 7. CHAKULA

Kama zilivyo shule zote za bweni za serikali, Shule ya Sekondari Lindi Wasichana hutoa chakula safi na salama ambacho huliwa na watanzania wote, ambacho Serikali inapendekeza kuliwa na mwanafunzi. Endapo unayo miiko au upekee ya kutokula vyakula fulani, tafadhali usipokee nafasi hii kwani shule haitatoa huduma ya pekee kwa kila mwanafunzi. Pia shule haitoi kibali kwa mwanafunzi kujipikia hivyo asilete vyombo vya kupikia au chakula kama mchele, unga, biskuti, mkate, kinywaji cha aina yoyote n.k. na haturuhusu mwanafunzi kununua aina yoyote ya chakula/kinywaji toka nje ya shule.

## 8. TAALUMA

Mwanafunzi ni lazima ahudhurie vipindi vyote vya masomo na kufanya mazoezi yote anayopewa na mwalimu wa somo husika. Asipofanya hivyo atapewa adhabu ikiwemo kurudishwa nyumbani.

Kila mwanafunzi anatakiwa apate alama zisizopungua **50/100** kwa kila somo Akishindwa kufikisha alama hizo kwa somo lolote hataruhusiwa kwenda likizo.

## 9. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.

Shule ya Sekondari Lindi Wasichana inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais –TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku(Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- ❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- ❖ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).**

**10. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWA NAFUNZI AFUKUZWE SHULE.**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule (twende kilioni nywele 5 hadi 7).
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uvutaji wa sigara;
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xi. Kusababisha mimba;
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**11. NGUO NYINGINE**

Mwanafunzi aje na khanga au kitenge doti moja, gauni au sketi ndefu mbili (02) kwa wataoshona sare shuleni. Mwanafunzi atakayeshona sare nyumbani aje akiwa amevaa sare za shule. Mwanafunzi anaruhusiwa kuvaa Track Suit wakati wa kujisomea (prep) ya jioni ili kuzuia mbu. Kinyume na hapo atarudishwa nyumbani kurejesha nguo zisizotakiwa kwa gharama zake.

***Masanduku/mabegi makubwa hayaruhusiwi, kwani hatuna nafasi ya kuyatunza. Akija nalo atalazimika kurudisha kwa gharama zake.***

## 12. MAELEZO YA ZIADA KWA MZAZI/MLEZI

(i) Shule inafuata mihula inayotolewa na Wizara ya Elimu Sayansi Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi, hivyo inakuwa na mihula mirefu miwili na mifupi miwili kwa mwaka. Mzazi /mlezi unaombwa kutoa ushirikiano wako kuhakikisha mtoto anawasili kwa wakati shuleni, vinginevyo sheria itachukua mkondo wake.

(ii) Mawasiliano yoyote kati ya mwanafunzi na mzazi/mlezi yafanyike kupitia Mkuu wa shule, Makamu mkuu wa shule na ofisi ya Malezi. Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na simu ya mkononi awapo shuleni.

(iii) Shule haina utaratibu wa kuwaona wanafunzi isipokuwa mzazi ataitwa na uongozi wa shule kama kuna ulazima wa kufanya hivyo.

(iv) Aidha unashauriwa kutomruhusu mwanao kumiliki simu kipindi hiki ambacho umri wake unampa shida kuyatawala mazingira ya utandawazi.

(v) Mzazi/mlezi kutompa mtoto fedha nyingi ambazo zitamfanya apoteze utulivu wa akili na kuvunja sheria za shule.

(vi) Shule ina utaratibu wa kushughulikia usafiri kwa wanafunzi wanaotoka mbali kipindi shule inapofunga. Hivyo mzazi/mlezi utapewa taarifa kabla ya shule kufunga.

(vii) Mzazi hakikisha unapima afya ya mwanao kwa uaminifu ili kuepuka usumbufu wakati wa masomo.

(viii) **Iwapo mwanao ana ugonjwa unaomsumbua mara kwa mara, tafadhali aje na vyeti pamoja na dawa anazotumia na akabidhi kwa Muuguzi wa Shule. Hii itarahisishia shule kumhudumia. Usipofanya hivyo shule itashindwa kumhudumia. Usifiche ugonjwa, utapokelewa tu, kupata elimu ni haki yako.**

(ix) Mwanafunzi anaruhusiwa kuleta pasi ya mkaa kwa ajili ya kunyooshea nguo zake. Ni marufuku mwanafunzi kuwa na kutumia pasi ya umeme amakifaa chochote kinachotumia umeme. Akibainika hatua kali zitachukuliwa dhidi yake ikiwemo kusimamishwa shule.

(x) Shule itakapokuwa imefunga, likizo zote **mwanafunzi atatokea shuleni moja kwa moja kwenda kwa mzazi wake (nyumbani kwao) na shule itakapofungua atatokea nyumbani kwao (kwa mzazi) moja kwa moja**

**kuja shuleni**. Atakayekiuka utaratibu huu atarudishwa nyumbani kwa gharama zake.

## 13. VIAMBATISHO NA FOMU MAALUM

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;

ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;

iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

## PICHA YA MUONEKANO WA SHAMBA DRESS





## MUONEKANO WA SKETI KWA MBELE NA NYUMA



**MINISTRY OF PRESIDENT'S OFFICE, REGIONAL ADMINISTRATIONS AND LOCAL GOVERNMENT**

Lindi Girls Secondary School
P.O BOX 1070
LINDI.

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**.

Please examine Miss

………………………………………………… as her physical and mental fitness for admission as a form …………………… Students at Lindi Girls' Secondary School in the year ………………

Your sincerely.

HEADMISTRESS

The headmistress,

I have examined Miss ……………………………………………………… as shown and consider that she is physically and mentally fit/unfit for admission to pursue a full-time secondary school education.

1. Vision with/without glasses. Right ……………………… Left ………………………
2. Blood pressure …………………………… Hemoglobin ……………………………
3. Hearing ……………………………………………………………………………
4. Urine (a) Albumen………………………… (b)...........................................
5. ( a) Venereal diseases…………………………(b) Bilharzia ............................
6. Pregnancy ………………………………………………………………………...
7. Neurosis……………………………………………………………………………
8. Is there any abnormality of : ( a ) The heart………………………………………

   ( b) Lungs…………………… (c) The spleen ……………………………………………
9. Are there serious diseases. E.g. Leprosy, Epilepsy, Asthma, Diabetes, etc.

Date …………………………… Signature of the medical Officer ……………

Station ……………………… Designation …………………………...

**SHULE YA SEKONDARI YA SEKONDARI YA LINDI WASICHANA**

**FOMU MAALUM INAYOONYESHA TAARIFA ZA NDUGU WA JIRANI NA MWANAFUNZI**

Ndugu wa karibu na mwanafunzi: Hakikisha unaandika majina matatu na anwani zao. Hii inasaidia shule kutoa taarifa endapo tatizo litatokea . Hatutaki majina ya ndugu wa bandia.

1. (a) Jina:_____________________________________________________________

   (b) Uhusiano:_______________________________________________________

   (c) Anwani:___________________________________________________________

   (d) Namba ya Simu:__________________________________________________

2. (a) Jina:_____________________________________________________________

   (b) Uhusiano:_______________________________________________________

   (c) Anwani:___________________________________________________________

   (d) Namba ya Simu:__________________________________________________

3. (a) Jina:_____________________________________________________________

   (b) Uhusiano:_______________________________________________________

   (c) Anwani:___________________________________________________________

   (d) Namba ya Simu:__________________________________________________

Saini ya mzazi: ______________________

Tarehe: ____________________________

**YAH: AHADI YA KUTEKELEZA WAJIBU**

Mimi ________________________________________nakubali nafasi niliyopata katika Shule ya Sekondari ya Lindi Wasichana, kuendelea na masomo yangu. Nafahamu ninagharamiwa na Taifa linadhamini kazi na juhudi. Naahidi mbele ya mzazi/mlezi wangu kuwa nitajitahidi upeo wa uwezo wangu kuwa mwanafunzi mwema. Naahidi nitashirikiana na Walimu, Wafanyakazi wasio walimu pamoja na wanafunzi wenzangu katika kila jambo lenye manufaa kwa Shule na Taifa kwa ujumla.

__________________

Saini ya mwanafunzi

Mimi ______________________________________ nimesoma yote na kuelewa . Naahidi kwamba nitampatia mahitaji yote kama ilivyoagizwa katika barua. Ripoti zote zinazomhusu Binti yangu zitumwe kwa anwani ifuatayo:

___________________________________________

___________________________________________

___________________________________________

___________________________________________

Jina na Saini ya mzazi/mlezi:

____________________________________________________________________

Tarehe: _____________________________